# TANZU NA FANI ZA FASIHI SIMULIZI

M.L. Balisidya (Matteru)

Tanzu ni nini? Tanzu ni neno linalotumiwa kumaanisha tawi, katika mazungumzo ya kawaida. Kwa maana hiyo hiyo tunaweza kuona kuwa fasihi simulizi ina matawi yake. Matawi haya tutayaita tanzu (wingi) utanzu (umoja). Tanzu katika fasihi humaanisha aina au fungu la tungo za fasihi zenye vigezo vya muundo na mbinu za uwasilishaji za aina moja au zinazofanana. Yaani tungo zenye fani ya aina moja.

Kwa mujibu wa maelezo haya, fasihi hugawika katika tanzu mbalimbali. Mgawanyo huu tunaweza kuupata kutokana na uchunguzi wa kitaaluma; lakini pia mgawanyo huu umo katika matumizi ya kawaida ya watu. Ni kweli kuwa katika matumizi ya kawaida, vigezo vya kuzipambanulia tanzu hizo ni tofauti kidogo na vile vya kitaaluma.

Ndani ya utanzu mmoja wa fasihi kuna fani (aina) mbalimbali. Neno fani (kwa maana ya pili) linazingatia aina au fungu dogo zaidi ya utanzu, la tungo zenye mwendo na mbinu za utoaji za aina moja. Wa aidha zenye wadhifa na dhamana ya aina moja.

Ni kweli kuwa wapo wanataaluma wengi ambao huchanganya matumizi ya maneno haya mawili tanzu na fani kuwa na maana moja katika taaluma hii. Tuchukue mfano dhahiri: Kimuundo hadithi ni tungo za fasihi za masimulizi zitumiazo lugha ya nathari (lugha ya ujazo, ya maongezi, ya kila siku) masimulizi haya hupangwa katika mtiririko wa vituko unaokamilisha kisa. Ili kisa hiki kikamilike hadithi huwa na wahusika ambao ndio nyenzo ya kukiendeshea kisa chenyewe, vivyo hivyo hadithi huwa na maudhui

Hayo ndiyo mambo ya msingi katika kuitambua hadithi. Lakini zipo hadithi za aina mbalimbali; nazo hutofautiana katika vipengele fulani fulani. Mathalani zipo:-

(a) Ngano: "Hadithi za paukwa pakawa ... wakaishi raha mstarehe" aghalabu zina nyimbo. Kwa kawaida ni hadithi za maadili ambazo husimuliwa katika mazingira ya starehe; nazo huadili kwa kutumia istiara, kharafa, hekaya n.k. Huwa na wahusika wa aina mbalimbali: wadudu, wanyama, binaadamu, mizimu, na miungu.

Wa aidha viumbe visivyo na uhai kama: Mawe, Miamba n.k. Wahusika hawa hupewa urazini wa binaadamu, ili kuadilisha.

(b) Tarihi: Hizi ni hadithi ambazo husimuliwa juu ya matukio ya kihistoria. Matukio haya huweza kuwa ni ya kweli ila hufumwa katika sanaa yenye ubunifu ndani yake kwa kadri ya kuupeleka ukweli katika masafa fulani kutoka kwenye sanaa. Mara nyingi wahusika wake ni binaadamu; ila hawa hupewa uwezo mkubwa au mdogo mno kuyakinisha matukio na kuyawekea mantiki.

(c) Visasili: ni hadithi ambazo pamoja na kuwa na wahusika wa aina mbalimbali, hasa Miungu na Binadamu, husimulia juu ya matokeo ya kiada. Hujaribu kuieleza miviga, imani na dini, za jamii. Aghalabu hadithi za aina hii hutambwa mivigani.

Pengine zipo fani zaidi ya hizi katika utanzu huu wa hadithi ambazo zinangojea kufanyiwa uchunguzi. Mathalani Wagogo wana hadithi fupi fupi ambazo hutumiwa katika maongezi yao, nazo hutumiwa kama mifano. Hadithi hizi zinaweza kutokana na matukio ya kweli au ya kubuni. Mwanzo na mwisho wake hutegemea maongezi. Hadithi hizi huitwa Mbazi (yaani methali). Yapo pia makabila mengine ya Kiafrika yanayotambua kuwepo kwa hadithi za aina hii. Nao huziweka katika fungu hilo hilo (la methali)!

Katika fasihi simulizi ugawanyaji wa tanzu na fani zake si wa moja kwa moja. Kwa ajili ya utendaji na uwasilishaji wake ni vigumu kuzifunga tanzu hizo kubakia katika hali moja. Tanzu na fani za fasihi simulizi huingiliana. Wimbo huweza kuwa hadithi na hadithi kuwa methali na methali kuwa kitendawili. Mifano michache itadhihirisha hali hii:-

Mfano wa Kwanza:

(a) Hasira Hasara! (Methali)?
(Msemo)

(b) Hasira Hasara! (Kitendawili)
(Jawabu: jani la mgomba).

Mfano wa Pili:

Kuna methali, kwa Wagogo, isemayo "Kula kwingi kulimchelewesha nyoka, akakosa miguu."

Pia kuna hadithi inayoeleza jinsi Nyoka na Wanyama wengine walivyoalikwa Nyumbani kwa Mfalme kwenye sherehe. Kule walikula na kula! Baadaye Mfalme aliwaita wapewe zawadi: Nyoka kwa ajili ya uroho hakusikia wito. Alipozinduka alikuta miguu yote, hata ile hafifu ya buibui na tandu, imeshatolewa. Akabakia anaburuzika kwa tumbo lake.

Hata hivyo, tanzu na fani mbalimbali za fasihi simulizi zinaweza kugawanywa, (kwa kusadifu matumizi tu) kufuatilia mtindo wa lugha iliyotumiwa kuziwasilisha. Kwa hiyo tanzu na fani zote zitaingia katika mafungu matatu ya mitindo ya lugha, katika fasihi simulizi: nathari, ushairi, semi.

(a) Nathari: Ni fungu linalojumlisha tungo zote za fasihi simulizi zenye kutumia lugha ya kawaida ya maongezi - lugha ya ujazo. Katika lugha hii ya maongezi, mapigo ni huru, hufungamana na yale yanayotumiwa katika mazungumzo ya kawaida. Kwa hiyo tungo zote za masimulizi zimeingia katika fungu hili: masimulizi yanayotumiwa katika miviga, ada na pia katika mazingira mengine ya kawaida. Kwa maelezo haya, nathari hujumlisha tanzu na fani zifuatazo; hadithi: Ngano, Tarihi, Visasili, Methali (Vigano) na masimulizi: utani na soga.

(b) Ushairi: Ni fungu linalojumulisha tungo zote za fasihi simulizi zenye kutumia Mapigo kwa utaratibu maalum: Mapigo ya kimziki, mathalani mapigo hayo yanaweza kupangwa kwa muwala wa urari ifuatavyo:

Ukipata Sikuoni, yote huubalikia
Basi mimi samahani, Uende nimegutuka (8,8)
Hunipati asilani, Jua nimeerevuka (8,8)

ama mapigo hupangwa kufuatia mapigo ya kazi; mdundo wa ngoma au ala nyingi za muziki makofi na miondoka ya uchezaji. Mfano mdogo wa kighani cha watoto utasadifu:-

Watoto wa Mjini,
Wamezoea,
Wakiona Disco,
Wanadoea,
Wakiulizwa nini?

Nataka Mdundiko

Mdundiko

Mdundiko

Havinitishi, tishi, tishi
Havinibabaishi, ishi, ishi,
Ule Mpango vipi,

Vipii?

Vipii?[3]

Hakuna urari katika mapigo ya utungo huu, lakini hatuwezi kusema kuwa utungo huu ni maelezo ya kawaida, kutokana na jinsi mapigo yake yalivyotengwa na yale ya maongezi ya kawaida. Utungo huu umetumia mapigo yaliyo huru, lakini yanayoambatana na uchezaji na mahadhi ya utongoaji. Basi tuseme ushairi hutumia mapigo yanayoleta hali ya muziki.

Vile vile katika ushairi kuna mkato wa lugha, na matumizi ya lugha kwa mpangilio mahususi. Nyimbo na vighani mara nyingi hutumia maelezo ya muhtasari na yenye kuachana na sarufi na mpangilio wa lugha wa nje na wa kila siku. Muhtasari wa maelezo huweza kufikiwa kwa njia mbalimbali. Kuu katika ya njia hizo ni ile ya tamathali, picha na ishara. Tuone mfano ufuatao:-

Sare, Sare, Maua!
Asiyejua kuchagua!
Kabila yake Mzigua!

Sentensi ya kwanza haisemi kitu hivyo ilivyo; lakini ambayo inatoa wazo la uzuri na mfanano wa watoto-wasichana-maua. Ua limekusudiwa kusimamia uzuri hapa. Kutokana na ibara ya matumizi ya utungo ni uzuri wa watoto waliopendeza kama maua kwa kuvaa sare.

Sentensi zifuatazo zinasisitiza uzuri wa watoto kwa kuweka utani:

Asiyejua Kuchagua!
Kabila yake Mzigua!

Yaani watoto wote ni wazuri, wote wanafanana atachaguliwa yupi? Na atakayeshindwa kupata chaguo lake astahili kuchekwa: ni Mjinga(?)

Pamoja na ushairi kuwa na mapigo ya kimuziki, mpangilio maalum wa maneno na mkato wa maelezo, ushairi huwa na ladha katika mlio. Mlio uletao ladha katika

ushairi huweza kupatikana kwa njia nyingi; moja kuu ni ya kutumia vina. Katika utungo wa hapo juu ua imetumiwa kuleta ladha:

Maua asiyejua kuchagua
Kabila yake mzigua

Katika mfano mwingine wa kilugha mlio kama huu waweza kupatikana:

Si nali Mtembedzi
Je si kuwa matembezini

Mdzelelo yakulonga dzo utodzi
(Wakati) kijana amezungumzia ndoa!

Mhindza Mwana nhendu gwe
Binti ya fulani loo

Mswanu Wadzelelo.
Mzuri bila kifani.

Wali wuye bito kawalonjele
Ungerudi uende uwaeleze

Wayetu Mdze'lo yasimbile
Wenzetu kijana amenuna

Mhindza Mwana nhendu wadzelo
Msichana, binti fulani vijana

Wamwisajaga uje uje ...
Humjivunia kweli kweli ...

Wakati mwingine mlio hupatikana kwa kutumia takriri, tanakali, na mrudio rudio wa maneno. Mifano imo katika nyongeza. Pamoja na hayo yote ushairi huwa na maudhui (yawe mepesi au mazito).

Ushairi hujumlisha nyimbo na maghani ya aina mbalimbali. Katika Ushairi tanzu muhimu ni zifuatazo: Nyimbo na Maghani;-

(i) Nyimbo ni tungo za kishairi zenye kutumia mahadhi, melodia, mkongosio, mapigo na muwala. Nyimbo huweza kuimbwa na mtu mmoja pekee ama na wazumi wake, wakiitikia mkarara. Zipo nyimbo za fani mbalimbali: Bembea, tumbuizo, tahlili, za ngoma, za mivigani, za michezo, za siasa za kawaida n.k. (Nazo hapa kwetu huchukua majina tofauti kufuatana na jamii).

(ii) Maghani ni tungo za kishairi zilizokusudiwa kutongolewa bila ya kutumia melodia wala mahadhi yo yote. Bali hutongolewa kwa kutumia sauti kati ya Uimbaji na Uzungumzaji ukisisitizwa utumizi wa mapigo unaoleta mwendo na kasi inayohitajika. Kiimbo (cha sauti) huwa ni muhimu katika kutia ladha na hata maana. Wakati mwingine kiimbo kisicho kwenda juu wala chini. Pahali pengine sauti ya juu na chini katika kiimbo imetumika kuleta ladha na uzito wa maana. Mifano iliyotolewa ya "Watoto wa Mjini" na "Sare Sare Maua" inaweza kueleza wazo hili.

Katika utanzu huu wa maghani zinaingia fani nyingi za kishairi zinazotongolewa, kama vile: Majigambo, vighani vya watoto, vya michezo, vya kazi n.k.

(c) Semi: Ni fungu la tungo za fasihi simulizi ambazo ni fupi fupi zenye kutumia picha, tamathali na ishara. Aghalabu ni mafumbo yanayokusudiwa kubeba maudhui yenye maana zinazofuatana na ibara mbalimbali za matumizi:

(i) "Mke ni Nguo, Mgomba kupaliliwa."

Picha ya Mgomba na Nguo zimetumiwa kusimama sambamba na ile ya Mke. Katika methali hii imani ya kuwa mwanamke ni kiumbe mnyonge na anayehitaji kutunzwa ili awe na manufaa zaidi inajitokeza.

(ii) "Vizee vyangu viwili kutwa vinatwanga" (Kope)

Katika kitendawili hiki, fumbo lililomo limetolewa kwa njia ya picha ya vizee ambavyo vinafanya kazi tokea mawio hadi machweo. Bila shaka Jawabu lake linataja kitu dhalili, dhaifu, kinachofanya kazi bila kupumzika mchana kutwa - kope.

Fungu la semi lina tanzu dhahiri zifuatazo:-

Methali:- Misemo itumiwayo kueleza kitu kwa njia ya picha na kwa ufupi ili itoe adili au onyo fulani. Aidha ili kusifu n.k. Misemo hii humithilisha maisha kwa njia ya tamathali, picha na ishara. Kwa mfano tu;

"Mtoto wa Nyoka ni Nyoka,"

fani zinazoweza kujitokeza hapa ni misemo na nahau

<u>Vitendawili</u>:- Mafumbo ya kuchemsha bongo ambayo hutolewa jibu maalum. Mafumbo haya hutumia picha, tamathali na ishara. Kwa mfano: Tseh! (Jibu-Sindano). Fani zinazoweza kuingia katika utanzu huu ni kama vile:- Mizimu (ya jando) na mafumbo. Mizimu ni semi zinazotumika katika ada za upisho ili kutoa mafunzo. Zinatumika katika nyimbo na maongezi. Mifano ifuatayo ni Mzimu:-

- Miti yote nitapanda mtalawanda Wanishinda!
- Muyujiyuji Mti wa Majini, hata ustawi haujengewi nyumba![6].


<u>Misimu</u>: ni semi ndogo ndogo za kupita ambazo huzushwa katika mazingira fulani halafu hufa baada ya mazingira yale kutoweka. Semi hizi aghalabu ni za kitamathali;
Kwa mfano:-

(a) Tamtam mahonda ukinila utakonda!

(b) Kivumbi cha Mwanamakumbi (cha Mzungu na Mmatumbi kupigania kumbikumbi).

(c) Maskini zumbukuku mambo yako huku, kulia na machozi pukupuku!

Fani zinazojitokeza hapa ni nyingi kwani ziko ukingoni mwa eneo la fasihi kuelekea katika lugha ya kawaida. Kama tulivyoona katika haya mafungu matatu mna tanzu mbalimbali za fasihi simulizi ambazo, kama tulivyosema, kila moja yaweza kuwa ni mkusanyo wa fani mbalimbali zenye wasifu wa aina moja wa muundo na mbinu za uundaji. Lakini itabidi tutoe tahadhari kuwa mgawanyo wo wote wa tanzu na fani si kuwa ndiyo kauli ya mwisho. Katika mgawanyo huu kuna tatizo la ugiligili wa fasihi simulizi ambao huileteleza fasihi kugeuzika na kubadilika kwa kila utendaji. Kwa mujibu wa haya, upo mwingiliano katika tanzu na fani hizi ambao huweza kutokea wakati wo wote. Mwingiliano huu hufanya baadhi ya jamii kuwa na jina moja tu kwa fani zaidi ya moja. Mathalani jamii nyingi hawatofautishi ngano na visasili, ingawa wanatenga tarihi. Wagogo, kama mfano tu, huhesabu hadithi hizo za aina mbili kuwa ni simo, na zile tarihi kuwa <u>nghomo</u>[5]. Kisha zile za mifano wao huziita mbazi (methali).



FASIHI SIMULIZI
NATHARI
USHAIRI
SEMI
NGANO
TARIHI
VISASILI
NYIMBO
MAGHANI
VITENDA-WILI
Methali
MISIMU
Istira
Hekaya
Kwa nini na kwa namna gani?
Kharafa
Kumbukumbu
Shajara
Hadithi za Historia
Epiki
Kumbukumbu
Tenzi
Kwa nini na kwa namna gani?
Tahlili
Bembea
Tumbuizo
Ngoma
Mwiga
Watoto
Kwaya
Majigambo
Vijighani
Shajara
Tenzi
Kitendawili
Mizimu
Mafumbo
Msemo
Nahau
Utani
Masaguo
Soga

BIBLIOGRAFIA


1. Ben Amos, D. (1975) "Folklore in African Society" Research in African Literature Vol. 6. No. 2., fall, pp. 167.

2. Fatma Hani na Black Stars, (1980) Tanga.
*-U- ni Mzani unaoongezwa katika uimbaji ili kuleta urari wa mizani 8.

3. Kutoka Dar es Salaam: Mwenge, Buguruni, Tandika 1980-81.

4. Finnegan, R. (1970) amezigawa nyimbo na ushairi kwa jumla katika mafungu matano - Nyimbo: za watoto, za kazi, za kawaida, za siasa, na za miviga, katika Oral Literature in Africa O.U.P., London.

5. Kwa maelezo ya M.L. Balisidya, (1977) "Mabadiliko katika fasihi simulizi ya Wagogo." Tasnifu M.A. Chuo Kikuu cha DSM.

6. Misimu hii miwili inaweza kupatikana miongoni mwa fasihi simulizi za Wagogo, Wakaguru, Waluguru, na Wazigua, pia na Wasambala.

7. Ben Amos, D. 1975: Kama hapo juu Uk. 167 - 198.